HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.
MWANZA

TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 05/ 11 /2018 MWAKA WA FEDHA 2018/2019

1.0. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka.

Hivyo taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya matokeo ya Darasa la saba mwaka 2018
ii. Taarifa ya maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha Kwanza mwaka 2019
iii. *Taarifa ya ziara ya Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI*
iv. *Taarifa ya ya uejzi wa Hospitali ya Wilaya*
v. *Taarifa ya Kupokea visima 7 vya Maji*

2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

2.1 *Taarifa ya Matokeo ya Mtihani ya Darasa la saba 2018*

Mhe Mwenyekiti, Mnamo tarehe 3 /09/2018 hadi 06/09/2018 Wanafunzi wa darasa la saba katika Halmashauri yetu walijumuika na wanafunzi wengine katika nchi yetu kufanya mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba. Katika mtihani huo jumla ya wanafunzi 8,420 kati ya wanafunzi 8,882 wamefaulu ambayo ni sawa na asilimia 94.80. Aidha, jumla ya wanafunzi 463 ambayo ni asilimia 5.2 hawakufaulu mtihani huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayofuraha kulijulisha Baraza lako kuwa, Halmashauri yetu katika mtihani huo imeweza kushika nafasi ya 6 kati ya Halmashauri 186 Tanzania Bara. Pia imeweza kushika nafasi ya kwanza Kimkoa kati ya Halmshauri zote 8 zilizopo ndani ya Mkoa wa Mwanza. Kupitia mafanikio haya, tunawanpogeza Idara ya Elimu Msingi kazi nzuri waliyofanya na wadau wote kwa ushirikiano walioonesha na kuiwezesha Halmashauri Kufikia mafanikio haya.

2.2 *Taarifa ya Maandalizi ya kuwapokea kidato cha Kwanza kwa mwaka 2019*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina jumla ya Shule za Sekondari 46, Shule za Serikali ni 24 na Shule zisizo za serikali 22. Takwimu za mwaka huu 2018 Wilaya ina jumla ya wanafunzi 21,966 kwa shule za Serikali. Idadi ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne Novemba mwaka huu ni 3,424 ambapo wataacha vyumba wazi 86 baada ya kumaliza.
Hata hivyo Halmashauri inatarajia kupokea wanafunzi 8,420 wa kidato cha kwanza, watakaohitaji vyumba 210. Ukiondoa vyumba 86 vitakavyoachwa na wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne mwaka huu, Halmashauri itakuwa na mahitaji mapya ya vyumba vya Madarasa 669, vilivyopo 345 na upungufu 324 na mahitaji ya viti na meza ni 26,742 vilivyopo 16,212 na upungufu utakuwa 9,883.

Mikakati ya kukabiliana na upungufu wa miundombinu ya shule za sekondari

1. Halmashauri imeziandikia WDCs zote kuzijulisha mapungufu ya Miundombinu ya shule katika kata zao ili waweke mipango ya kukabiliana na changamoto hizo za upungufu.
2. Halmashauri inaanda kikao cha wadau wa elimu ili kuandaa Mpango wa pamoja wa kukabiliana na changamoto hizo.
3. Halmashauri imewaagiza wakuu wa shule kufanya ukarabati wa viti, meza na Madarasa ilikupunguza upungufu wa miundombinu ya shule.
4. Kupita kwenye shule za Sekondari kutoa elimu na kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia gharama za ujenzi kwa wadau kama vile Wajumbe wa Bodi, Walimu, Wanafunzi, Wazazi na Wananchi wa kila Kata.

2.3 *Taarifa ya ziara ya Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 22/10/2018 Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alitembelea Wilaya yetu ambapo alipata nafasi ya kuongea na wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi na Watumishi. Aidha, Mhe. Waziri aliweza kukagua mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Barabara ya Buswelu – Kiseke – Sabasaba na kituo cha Afya Buzuruga.

Katika ziara hiyo, Mhe,. Waziri aliipongeza sana Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo na aliweza kuthibitisha kuwa miradi yote inayotekelezwa ina viwango na ubora wa hali ya juu. Pia aliipongeza Halmashauri ya Manispaa kwa kuweza kufunga mfumo wa ukusanyaji mapato na takwimu za sekta ya afya katika vituo vyote 16 vya kutolea huduma za Afya vilivyopo. Mfumo huu umewezesha kuongeza mapato ya vituo maradufu ikilinganishwa na mapato ya awali.

2.4 Taarifa ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 01/10/2018, Halmashauri yetu ilipokea fedha kiasi cha Tshs 500,000,000 kati ya Tshs 1,500,000,000 zilizotengwa katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali ya wilaya. Ujenzi huu utaanza mara moja mara baada ya kupokea maelekezo kutoka TAMISEMI.

Pia Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeanza ujenzi wa kituo maalumu cha magonjwa ya mlipuko hususani Ebora (isolation centre) katika eneo la Hospitali ya Wilaya. Aidha, mradi huu unatekelezwa moja kwa moja na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee.

2.5 Taarifa ya kukabdhidhiwa visima 7 vya Maji

Mheshimiwa Mwenyekiti; Halmashauri, Mhe, Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe. Dkt. Angeline S.L Mabula kwa kushirikiana na Taasisi ya Kiislam ya Afrika (Africa Muslims Agency) imefanikiwa kutekeleza mradi wa kujenga visima vifupi 7 Awamu ya kwanza, ujenzi huu ulianza Mwezi Julai 2018 hadi Oktoba 2018 na kutekelezwa kwa 100% katika mitaa ya Chabakima, Masemele, Ilalila, Bulyanghulu, Isanzu, Kadinda, na Kimanilwentemi. Visima vyote hivi vimegharimu **Tshs 28,000,000**.

Hivyo naniyofuraha kulijulisha baraza lako kuwa, mnamo tarehe 3 - 4/11/2018 visima vyote vimekabidhiwa rasmi katika mitaa husika ili waendelee na uendeshaji.

Awamu ya pili mradi huu utaendelea katika uchimbaji wa visima virefu 7 vingine katika maeneo ya shule ya msingi Kabusungu, Masemele, Kilabela, Shule ya Sekondari Shibula, Mtaa wa Ibinza, Lukobe na Mtaa wa Ibaya. Ujenzi huu wa visima virefu utaanza mara baada ya utafiti wa maji chini ya ardhi kukamilika.

Aidha tunamshukuru Mhe. Mbunge na Taasisi ya Kiislamu kwa Afrika (Africa Muslims Agency) kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuendeleza mapambano ya kumtua ndoo kichwani mama wa Ilemela.

Naomba kuwasilisha

John P. Wanga
Mkurugenzi wa Manispaa
ILEMELA